

## **Hali ya VVU / UKIMWI nchini Ethiopia**

### **Imeandikwa na Janet Otsuki**

Shirikisho la Jamhuri ya kidemokrasia ya Ethiopia ni nchi katika afrika mashariki inayopakana na bahari na kusini mwa bahari ya kanda. inapakana na Sudan magharibi, Eritrea kaskazini, Djibouti na Somalia mashariki, na Kenya upande wa kusini. Taifa hili lina majimbo tisa ya huru.

Ethiopia ni nchi ya kipekee miongoni mwa nchi za Afrika kwa kuhifadhi uhuru wake kutoka utawala wa kikoloni licha ya miaka mitano ya uvamizi wa Italia. Hata hivyo, nchi hii ina historia ya hivi karibuni ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, kisiasa, ukandamizaji, rushwa za kisiasa, na haki za binadamu. Tishio kubwa la usalama wake ni mgogoro wa mpakani na Eritrea uliomalizika bila mwelewano mwaka 2000 na watu 70,000 kupoteza maisha.

Katika masuala ya afya na ustawi wa jamii, Ethiopia inajumuika kati ya mataifa maskini zaidi duniani. Karibu nusu ya watu milioni 77 wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi. Ripoti ya Umaskini ya Binadamu ya 2004 kwa nchi zinazoendelea inajumuisha Ethiopia 98 kutoka mataifa 102. Taarifa za Oxfam ni kuwa utapiamlo wa watoto ni wa juu zaidi duniani na ukosefu wa usalama wa chakula ni mkubwa na wa muda mrefu.

Uchumi wa Ethiopia unategemea msingi wa kilimo unaotegemea mvua na kuchangia nusu ya jumla ya bidhaa za ndani na asilimia 60 ya mauzo ya nje. Kahawa ndio zao muhimu sana, lakini bei ya chini na huumiza wakulima. Zaidi ya hayo, udongo kuishiwa nguvu na ukame ni pigo kali katika sekta ya kilimo.

### **Mgogoro wa kitaifa**

Safu ya 2004 ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo ya Binadamu inajumuisha Ethiopia sehemu 170 kati ya nchi 177 duniani kote kutokana na sababu kadhaa; Moja ya hayo ni urefu wa maisha, ambao umeshuka hadi miaka 47.8 kutokana na uhaba wa chakula wa mara kwa mara, mapigano yanayoendelea, na janga la ukimwi.

Kesi ya kwanza ya VVU ilipatikana mwaka 1984, na kesi mbili za kwanza za UKIMWI ziliripotiwa mwaka 1986. Leo, janga la ukimwi ni mgogoro wa kitaifa nchini Ethiopia. Inakadiriwa watu 1.32-1,500,000 walikuwa wanaishi na VVU / UKIMWI katika 2005. Mwaka huo, kulikuwa na kesi 128,900 za maambukizi mapya ya VVU, kwa kiwango cha watu 353 kwa

siku. 30,300 ya hawa ni waliozaliwa na VVU.

Janga la UKIMWI sasa linatambuliwa kama sababisho kuu la vifo nchini Ethiopia. Katika mwaka wa 2005 kulikuwa na kesi 137,500 za maambukizi mapya ya UKIMWI na vifo 134,500 vya UKIMWI. Kulingana na mpango wa dharura wa rais wa Marekani kuhusu UKIMWI, idadi ya waliopotea kwa UKIMWI inakadiriwa kuwa jumla ya watu 900,000 kwa mwaka 2003 na inakadiriwa kufikia milioni 1.8 ifikapo mwaka 2008 kama mienendo ya sasa itaendelea.

Mambo kadhaa yanachangia maambukizi ya VVU katika nchi ya Ethiopia. Kulingana na Mpango wa pamoja waa Umoja wa Mataifa wa VVU / UKIMWI (UNAIDS) mambo haya ni kama; kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira, uhamiaji; kuenea kwa biashara ya ngono, ukosefu wa uwezo wa kusoma na kuandika; tofauti za kijinsia, madhara ya utamaduni na jadi, na unyanyapaa na ubaguzi kwa wale wanaoishi na kuathirika na VVU.

### **Uhaba mkubwa wa ajira**

Ukosefu wa ajira hasaa kwa vijana nchini Ethiopia ni mkubwa mno, asilimia 54, kwa mujibu wa Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF). Kiwango cha ukosefu wa ajira ni cha juu katika kundi la umri 15 hadi 19, kufuatiwa na kundi la umri 20- 24. wanawake wanajumuisha sehemu kubwa zaidid ya waliokosa ajira makundi haya.

Umaskini na ukosefu wa fursa za kujiendeleza unaweza kuharibu misingi ya jamii. Familia maskini zinanaweza kulazimishwa kushiriki makazi na wengine au kuhamia sehemu zingine ili kupata ajira. Uharibifu wa miundo jadi ya familia unaweza kusababisha upotevu wa hadhi katika jamii, kuongezeka kwa kuavya pombe na unyanyasaji wa wake na watoto. Haya yote huchangia katika uambikizi wa VVU.

Ukosefu wa ajira unajulikana kuchangia maamuzi ya maisha ya hatari kwa vijana. Kwa mfano, matumizi ya pombe na madawa ya kulevya na wapenzi wengi, tabia zinazowahadhirisha na VVU.

### **Uhamiaji**

Uhamiaji huongeza uwezekano wa kuambukizwa na VVU kwa wale wanaosafiri na kwa washirika wao wa nyumbani. Shirika la Kimataifa la Uhamiaji linasema kuwa wahamiaji hukabiliwa na kuvunjika kwa kanuni za kijamii na kiutamaduni ambazo zinaongoza tabia katika

jamii imara.

Hatari zinazochangia kuongezeka kwa VVU ni kama:

1. kutengwa kwa wanaouguza kutokana na unyanyapaa, ubaguzi na tofauti za lugha na utamaduni;
2. kutenganishwa washirika wa kawaida wa kimapenzi;
3. ukosefu wa usaidizi na urafiki;
4. hali ya kutokujulikana, na
5. ukosefu wa huduma za afya na za kijamii.

Asilimia 84 ya wakaazi wa Ethiopia ilikuwa ya vijijini kufikia 2005. Wakaazi hawa hukumbwa na ufukara, uharibifu wa ardhi na shamba zilizochooka, ukame wa mara kwa mara na njaa, na shinikizo la idadi ya watu kuongezeka. Wanawake wa vijijini hasa kutoka sehemu za Kaskazini hukumbwa na mambo ya kijamii na kitamaduni kama ndoa za utotoni, talaka, kifo cha mume na ufinyu wa ardhi. Mambo haya hulazimisha maskini vijijini kutafuta kazi katika maeneo ya mijini.

Mbali na maendeleo mijini kuleta fursa za ujenzi na kazi za msimu, mahitaji ya ajira bado ni makubwa. Uhamiaji wa mijini huongeza utumizi wa huduma na miundombinu ya mijini na unaweza kusababisha kuongezeka kwa ukosefu wa ajira, biashara ya ngono na kuomba omba katika miji mikubwa.

Askari na wafanyakazi wa ngono ni idadi ingine ya wahamiaji. Kulingana na taarifa ya National Intelligence Council, wakati mgogoro wa mpaka na Eritrea ulipomalizika, uhamasishaji ulisababisha kutawanywa kwa askari wanaouguza na wafanyakazi wa ngono nchini kote. Hili ni wimbi la kwanza la kusambaratisha inayoongozwa na UKIMWI baada ya kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Ethiopia katika miaka ya 1980.

Sababu hizi zimechangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU katika maeneo ya mijini ya Ethiopia kwa asilimia 10.5. Hii ni mara tano ya juu kuliko katika maeneo ya vijijini, kulingana na UNAIDS. Maambukizi ya VVU bado ni ya juu katika mji mkuu wa Addis Ababa, kutoka asilimia 14 hadi asilimia 16. Kulingana na taarifa za Madaktari Wasiokuwa na Mipaka, mji wa Humera unakumbwa na maambukizi ya juu hasa kutokana na idadi kubwa ya wafanyakazi wa msimu, askari na biashara ya ngono.

### **Kuenea kwa biashara ya ngono**

Kama ilivyo mijini, Addis Ababa ina biashara ya ngono ilioenea na kuhusishwa na mikahawa, baa, hoteli, klabu za usiku na majengo mengine inayohusika na wataalam tajiri au wafanyabiashara. Sensa ya 2002 ya Family Health International (FHI) iligundua kuwa maambukizi ya VVU miongoni mwa makahaba wa mijini ni zaidi ya asilimia 20 na asilimia 50 katika baadhi ya miji.

Umaskini uliokithiri hulazimisha wasichana kujihusisha na biashara ya ngono. Sensa ya FHI iliripoti kwamba asilimia 60 ya wafanyakazi wa ngono mjini walikuwa kati ya miaka 15 na 24. Uwezekano wa Wasichana yatima kushiriki katika biashara ya ngono ni mara tatu zaidi ikilinganishwa ya watoto wasio yatima, hii ni kulingana na Population Council.

Saa zingine wateja husita kutumia kondomu, kuweka wafanyakazi wa ngono katika hatari kubwa ya kuambukizwa VVU. Aidha, mashirika chache hutoa huduma kwa wafanyabiashara ya ngono na VVU / UKIMWI, matunzo na msaada.

### **Changamoto ya wasiojua kusoma na kuandika**

Katika miaka ya 1970, serikali ya Ethiopia ilizindua mpango kabambe ya mafunzo ya kusoma na kuandika uliofaidi watu wazima na watoto. Licha ya hayo, ujinga bado ni kikwazo cha elimu kwa umma kuhusu maambukizi na uzuizi wa VVU. United Nation Population Fund (UNFPA) inaripoti kuwa kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika kati ya wanaume wa Ethiopia umri wa 15 na zaidi ni asilimia 48. Kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika miongoni mwa wanawake ni asilimia 62.

Vijana wasioenda shule ni wako kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa VVU. Kulingana na taarifa za Wizara ya Elimu ya Ethiopia, katika 2002 uandikishaji wa watoto katika darasa la 1 hadi 10 ulikuwa wa asilimia 48-57 kwa wavulana na asilimia 37 kwa wasichana. Kwa mujibu wa UNICEF, elimu kwa vijana hupunguza uwezekano wa kukutana na hatari za afya ikiwa ni pamoja na VVU / UKIMWI, kulevya na vurugu.

Wazazi wengi wao hawana taarifa juu ya sababu za VVU / UKIMWI na hatari ya kukabiliwa na vijana wasichana. Matokeo yake, ni mara chache kujadili masuala ya ngono na watoto wao na jinsi ya kuepuka salama umwenendo

### **Jinsia**

Wanawake nchini Ethiopia, hasa vijana na wasichana, wako na kiwango cha maambukizi ya VVU cha juu kuliko wanaume. Ofisi ya Ethiopia ya Kuzuia na Kudhibiti VVU / Ukimwi inakadiri ya kwamba asilimia 55 au 730,000 ya watu wanaoishi na VVU / UKIMWI ni wanawake. Wanawake walichangia asilimia 54.5 ya vifo vya UKIMWI na 53.2 asilimia ya maambukizi mapya mwaka 2005.

Unyanyasaji dhidi ya wanawake ni sababu kubwa inayochangia kuenea kwa VVU. Ngono ya vita huchangia kuongezeka kwa hatari ya maambukizi ya VVU kwa sababu vidonda vinavyosababishwa hupitisha virusi vya ukimwi, hasa kwa wasichana wadogo ambao sehemu zao za uzazi hazijakomaa.

Vita vya kimwili na kingono ndani ya ndoa ni vya kawaida nchini Ethiopia. Utafiti wa mwaka 2005 wa Shirika la Afya Duniani (WHO) umebaini kwamba karibu theluthi moja ya wanawake wa Ethiopia katika kipindi cha mwaka mmoja waliripoti kulazimishwa na mpenzi kufanya ngono kinyume na matakwa yao.

Tatizo ingine ni ukosefu wa jinsi ya kujitetea na kujadili maswala ya ngono kati ya wanawake na wasichana wa Ethiopia, wengi wao hutegemea wanaume. Hawana mamlaka juu ya jinsi gani, lini na wapi ngono itatendeka. Wanawake wana ushawishi mdogo kuhusu ruhusa ya ngono na mpenzi au kujadili matumizi ya kondomu.

Wanawake pia hawana taarifa na jinsi ya kupata huduma za kujikinga na kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU. Hii ni kweli hasa katika maeneo ya vijijini, ambapo utamaduni na dini hutawala maisha ya wanawake na haki zao kupuuzwa. UNFPA inakadiria kuwa kati ya wanawake wa umri 15-24, asilimia 37 tu ndio wananjua kwamba mtu anaweza kujikinga na VVU kwa kutumia kondomu. Asilimia 63 ya wanaume wa umri huo hujua mbinu hii kuwa kweli.

Chanzo kikuu cha maambukizi mapya ya VVU miongoni mwa watoto, kwa mujibu wa UNAIDS, ni maambukizi ya mama kwenda kwa motto (MTCT) kutoka kwa mama wenye VVU kwa mtoto wake wakati wa mimba, leba, au kunyonyesha. Idadi kubwa ya kesi hizi huzuilika kwa njia ya tiba ya kurefusha maisha (ART). Hata hivyo, ushauri na matibabu duni nchini Ethiopia ina maana kwamba wanawake wajawazito wachache hupata huduma za kliniki na hata wachache zaidi kupata ARVs.

## **Madhara ya tamaduni**

Baadhi ya madhara ya vitendo vya kimila nchini Ethiopia ni ongezeko la hatari ya maambukizi ya VVU kwa wasichana na wanawake.

Mojawapo ya mila hizo ni kutahiriwa kwa wanawake, au tohara kwa wanawake. Kulingana na Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu nchini Ethiopia mwaka 2005, zaidi ya asilimia 74 ya wanawake wenye umri kati ya 15 na 49 wamefanyiwa aina fulani ya tohara. Tendo hili huongeze hatari ya mwanamke kupata VVU wakati wa ngono hasaa sehemu za uke zinapovunjwa kuruhusu kupenya. Jitihada za kukabiliana na vitendo zimekuwa na athari.

Ndoa za utotoni ni jambo la kawaida katika baadhi ya maeneo ya Ethiopia. Kulingana na sheria, umri wa ndoa ni 18, jambo linalopuuzwa kwa wingi. UNICEF inaripoti kuwa ndoa katika umri wa miaka saba au nane ni kawaida. Watoto hawa huzoeshwa ngono bila kondomu, huolewa na watu wazima, na hushindwa kujadili maswala ya ngono. Zaidi ya hayo, matatizo ya mimba za mapema huongeza hatari yakuambukiza magonjwa ya zinaa.

Mazoea mengine ambayo yanaweza kuongeza hatari ya maambukizi ya wanawake ni urithi wa wajane, ambapo mjane lazima aolewe na ndugu wa kiume wa marehemu mume wake. Jambo lingine ni ndoa kwa utekaji nyara, ambapo msichana hutekwa nyara na kundi la vijana na kubakwa na mtu ambaye anataka kumuoa. Wazee wa kijiji huuliza familia ya msichana huyo kukubali ndoa.

Serikali ya Ethiopia inajihamasisha kutokomeza aina zote za mila hatarishi. Inaunga mkono juhudi za mashirika yasiyo ya kiserikali kwa maswala haya ya mila, na mipango ya shule za serikali na kampeni za vyombo vya habari pia zinatumiwa kuzuia vitendo hivi.

## **Unyanyapaa na ubaguzi**

Wanaoishi na VVU/UKIMWI nchini Ethiopia hukabiliwa ba unyanyapaa na ubaguzi. Kulingana na Umoja wa Mataifa, kutovumilia huku huiimarisha chuki, ubaguzi na ukosefu wa usawa wa jinsia, umaskini, ulemavu na ukabila. Wanaotoka kwa makundi ya wachache husita kuwasiliana na afya na huduma za kijamii, hivyo kuwa hatarini ya kuambukizwa.

Kuzuia UKIMWI na matibabu ni muhimu kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya VVU / UKIMWI. Kulingana na UNAIDS na WHO, hatua muhimu katika mbinu hizi ni kulinda haki za watu wanaoishi na VVU/ UKIMWI na kutokomeza unyanyapaa na ubaguzi dhidi yao.

Nchini Ethiopia, ubaguzi pia husababisha watoto yatima kutengwa na kukosa makao. Mayatima

hawa hukabiliwa na kutengwa na jamii, ubaguzi na unyanyapaa na matatizo ya kihisia. Wao huwa na uwezekano mdogo wa kuchukuliwa na familia zingine au kupata ajira. Saa zingine mayatima wenyewe wanathirika na VVU.

Jumla ya watoto milioni 2.6 wamekuwa mayatima kutokana na janga la VVU / UKIMWI katika muongo uliopita. Makadirio ya UNCEF inaidadisha mayatima kuwa milioni 4.6, au asilimia 13 ya jumla ya idadi ya watoto. Idadi hii inakadiriwa kuongezeka hadi asilimia 14.8 mwaka 2010. Kama utabiri huu ni kweli, Ethiopia itakuwa na idadi kubwa zaidi ya watoto yatima duniani.

### **Juhudi za taifa za kukabiliana na VVU/UKIMWI**

Nchi ya Ethiopia imeongeza juhudi na jitihada za kudhibiti na kukabiliana na UKIMWI katika miaka ya hivi karibuni. Utulivu wa kisiasa na mbinu za kuhamasisha jamii zimeruhusisha mashirikiano ya sekta zote, ikiwa ni pamoja na vyama vya kiraia na jamii, sekta ya afya, na mashirika ya kimataifa.

Serikali ya Ethiopia ilizindua mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na janga la UKIMWI kupitia mkakati wa kitaifa wa miaka 2001-2005. Mwaka 2005, serikali ilizindua mpango mpya wa kwa ajili ya Kudhibiti VVU/UKIMWI wa miaka 2004-2008.

Mkakati huu unaongozwa na mbinu sita za kukabiliana na VVU/UKIMWI. Mbinu hizi ni kujenga uwezo; uhamasishaji wa jamii na ushirikiano na mipango ya afya; uongozi; uratibu na mitandao; na juhudi zinazolenga mambo maalum.

Shirika la kudhibiti na kuzuia VVU/UKIMWI (HAPCO) huratibu utekelezaji wa mikakati ya kila siku. Serikali ipo katika mchakato wa kupeleka mikakati yake chini ya Wizara ya Afya (MOH). Ushirikiano wa Taifa dhidi ya VVU/UKIMWI husaidia HAPCO kuratibu mipango na serikali, mashirika ya kiraia, sekta binafsi na wafadhili. Shirika la wafadhili huratibu shughuli za mashirika ya kimataifa na ya nyumbani. Donors' Health, Population and Nutrition Group huratibu misaada ya wafadhili katika sekta ya afya.

### **Changamoto**

Kulingana na UNAIDS, mafanikio kutokana na juhudi hizi ni duni sana ikilinganishwa na ukubwa wa janga la VVU/UKIMWI. Pia inaripoti mikakati ya serikali inakabiliwa na changamoto mingi.

Moja ya changamoto hizi ni kuendelea kuenea kwa janga maeneo ya vijijini. Nyingine ni uhaba

wa mahitaji na uhaba wa huduma, hasa katika maeneo ya vijijini. Mipango ya kutekeleza mikakati katika wilaya pia haitoshi. Mwisho, mipango imeshindwa kuleta mabadiliko kwenye jamii.

Elimu, tiba na msaada ni muhimu katika kuzuia maambukizi mapya na hivyo kuepuka ongezeko la maambukizi ya VVU. Kama ilivyoielezwa, wakazi wa vijijini hukosa mbinu kuzuia VVU, tiba, matunzo na huduma za msaada zaidi kuliko mijini maeneo. Idadi kubwa ya vijana iko hatarini, asilimia 34 ya vifo vyote vya vijana wa umri 15 hadi 49 nchi Ethiopia husababishwa na UKIMWI.

Wakazi walioathirika kwa wingi huhitaji umakini zaidi. Makundi haya ni pamoja na sekta ya usafiri, polisi, jeshi na wafanyabiashara ya ngono. Mipango ya elimu lazima kulengwa na mazingira maalum na changamoto za maisha yao. Taarifa na elimu inayolenga mazingira na hali zao ni bora zaidi kuhamasisha mabadiliko ya tabia.